# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**KABARAK HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# KABARAK HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/2**

**KARATASI YA PILI**

**(LUGHA)**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1**. Majibu ya Ufahamu.

1. Malengo manane ya nchi wanachama wa umoja wa mataifa,ambayo nchi hizi zilikubaliana kujizatiti kufikia mwaka wa 2016. (Alama 2)
2. Maskini ambao kipato chao ni cha chini ya dola moja kwa siku. (Alama 1)
3. i) Inaanzia shule ya chekechea hadi kidato cha nne. (Alama 2)
   ii) Ni ya lazima, yaani mtoto sharti ahudhurie masomo (Alama 1)
4. i) Kutohudhuria kliniki wakati wa kulea mimba.
   ii) Huduma kwa wajawazito kuwa mbali sana.
   iii) Namna za usafiri kuwa duni.
   iv) Kuhudumiwa na ‘wakunga’ wasiohitimu au hata kujifungua pweke.
   v) Ukosefu wa kinga muhimu na lishe bora. (zozote 3 alama 5)
5. Kwa kutumia vyombo vya habari na vituo tamba vilivyo na maafisa wa nyanjani. (Alama 2)
6. Kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu wanaoshindwa kupata maji safi na salama . (Alama 2)
7. i) ‘Hawazai njiti’ – Mimba hazitoki . (Alama 1)
   ii) ‘Vifo vya uzazi’- vifo vinavyotokea wakati kina mama wanajifungua. (Alama 1)

**2. <u>NIDHAMU</u>**

(a) Nidhamu (alama 1)

(b) Umuhimu wa nidhamu:

-Mwenye nidhamu ni nuru nyumbani hata shuleni.
-Anakuwa kiongozi wa wote / watu humtegemea
-Kiatu humpenda.
-Anajiepusha na shutalma na majanga.
-Kijumla anastahiwa.
-Hupata fursa ya kuteuliwa miongoni mwa wengi kwa dhima fulani.

(Hoja 6X 1 = alama 6, mtiririko al. 1, jumla alama 7)

(c) Muhtasari wa aya nne za mwisho.

i) Mwadilifu hajipati katika matatizo mengi.
ii) Lakini utovu wa nidhamu huanzia ututoni na mtoto huiga tabia za wazazi wake na huendelea shuleni.
iii) Utovu wa nidhamu hulipwa kwa adhabu mumu humu / watu wajirekebishe.

Makosa

| | |
|---|---|
| Sarufi | ½ x 10 = alama5 |
| Hijai | ½ x 6 = alama 3 |

Adhibu kila kosa la sarufi na hijai linapotokea

3. <u>MAJIBU</u>

a) Kipasuo, hafifu, hutamkwa katika kaakaa laini
b) “Maliza kazi hii haraka,” mwalimu alimwambia mwanafunzi.
c) Silabi funge huishia kwa konsonanti mfano
   Ma-k-ta-ba

d) U-i

A – wa

e) Walimu walikuwa wakiwaadhibu wanafunzi wenye hatia

f)

<table>
<tr><td colspan="9">S</td></tr>
<tr><td colspan="4">S1</td><td></td><td colspan="4">S2</td></tr>
<tr><td>KN</td><td colspan="3">KT</td><td>U</td><td>KN</td><td colspan="3">KT</td></tr>
<tr><td>N</td><td>T</td><td>T</td><td>KN<br>N</td><td></td><td>Ø</td><td>T</td><td>E</td><td>E</td></tr>
<tr><td>Omondi</td><td>anaazimia</td><td>kuwa</td><td>mhasibu</td><td>lakini</td><td></td><td colspan="3">Hatii bidii masomoni</td></tr>
</table>

g) Wanasafiri kwenda Marekani

h) Naomi atakupikia chai halafu aende kule uwanjani

mahali nafsi ya pili umoja

i) Riwaya yenye masuala ya kisiasa ni – kirai nomino
Watoto wa kike – kirai husishi

j) Koloni – hutenganisha jina la mhusika na maneno anayoyasema katika tamthilia
mfano
Mbua: Je alifika jana?
Hutanguliza orodha.mfano
Mama alinunua mboga : Nyama, nyanya na kitunguu.
Kistari kifupi (-)
Hutenganisha silabi za maneno
Kuonyesha neno linaendelea katika mstiari unaofuata baada ya kukosa kutoshea katika mstari
mfano
Ame-wasili

k) ni- kitenzi kishirikishi kipungufu
Wasiopendwa, wanaposema – vitenzi sabamba

l) Havikubaliki kama sentensi kamili
Hata kikiondolewa maana ya sentensi haipotei.
Hutambulishwa na vitambulishi vya utegemezi kama vile 'o' rejeshi

m) Amri

n) Hawala-Hundi / cheki
Katani – mkonge

o) Kitendo hakijatendeka na hakuna uwezekanao.

p) i) Walipewa soda na vile vile chupa
ii) Walipewa soda iliyokuwa kwenye chupa
iii) Walipewa soda iliyokuwa kwenye chupa

q) Jizi hili halikuiba jisu na gombe la jana jike lile

**4.ISIMU JAMII.**

a) Kiuchumi – maendeleo na ubunifu wa viwanda yanafanya watu kuhamia mijini .Watu wanapohamia mijini wanaacha kuzungumza lugha moja na kuanza kuzungumza nyingine kwa ajili ya mawasiliano

b) Uchache wa wazungumzaji – idadi ya watu wanaozungumza lugha fulani inapopungua lugha hiyo inakabiliwa na tisho la kufifia
c) Kutoungwa mkono na taasisi balimbali k.v elimu dini na vyombo vya habari hukabiliwa na tisho la kufa
d) Hadhi – lugha ambazo hazina hadhi kuishia kufa
e) Ndoa za mseto – watu wanapo changanyikana kupita ndoa za mseto husababisha lugha zingine kudidima
f) Kuhama kwa watu – kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine luga zao huadhiriwa
g) Sababu za kisiasa
h) Athari za elimu zozote 6x1

(b)

- Kiswahili kufanywa lugha ya Taifa / rasmi
- Katiba ilipitisha Kiswahili kiwe lugha rasimi nchini
- Kiswahili kufanywa somo la lazima shule za upili / msingi
- Shughuli za lazima bunge kuendelezwa kwa lugha ya kiswahili
- Vyombo vya mawasiliao kutumia lugha ya Kiswahili
- Vitabu vingi kuchapishwa kwa lugha ya Kiswahili zozote 4 x1